

East Africa Christian College, malengo yake makuu ni kuinua kiwango cha elimu na vipaji vya viongozi wa Kikristo kufikia kiwango cha uelewa Kimataifa.

Tunasaidia kuwaandaa Wanaume na Wanawake wawe viongozi watendaji bora watakaoweza kuleta mabadiliko mazuri ndani ya Mkanisa yao, ndani ya jamii na katika Nchi.

East Africa Christian College inalenga kuandaa moyo wa kiongozi - kiongozi aliyeko ndani, uwelewa wa kiongozi, uhusiano wake na Mungu na namna kiongozi anavyopaswa kutembea kwa busara ya mikono yake, ambayo ndiyo udhahirisho halisi wa huduma na uongozi.



Kozi mbalimbali

Kozi ni ya wiki moja (siku tano kamili) kukaa darasani kwa maelekezo na masomo, kazi za nyumbani (homework) na kazi zitakazofanyika nje ya darasa. Masomo mengine yataandaliwa kabla ya darasa na mwanafunzi anatarajiwa kumaliza siku ya kwanza ya darasa. Wengine watakuwa na kazi za kukamilisha jioni kwa maelekezo ya wiki na wengine watakuwa na kazi baada ya masomo na inatarajiwa kukamilishwa kabla ya kupokea shahada.

Kozi zitafundishwa na waalimu wahitimu ambao wanao ujuzi halisi wa kutenda yale wanayoyafundisha, hii pia inawajumuisha maprofesa kutoka America na nchi zingine za dunia.

Kozi zimeandaliwa kukuza, kufikiri kwa kiwango cha juu na kuwa na vipaji vya kutatua matatizo jambo ambalo ni la muhimu sana kwa viongozi wazuri.

Kukuza

MIOYO NA MIKONO

ya viongozi.



“Na Daudi akawalisha kwa ukamilifu wa moyo wake, na kuwaongoza kwa busara ya mikono yake.” ZABURI 78:72



Mpango

Certificate ya uongozi katika elimu ya Kikristo

Certificate ya uongozi katika elimu ya Kikristo ni mpango wa elimu ya mwaka mmoja (kozi itakuwa na vipindi 12) iliyoandaliwa kufundisha elimu ya msingi na vipaji vya huduma, kumwandaa mwanafunzi kwa elimu ya juu ama kwa ajili ya kuhudumia jamii. Iwapo mwanafunzi atafanya vizuri katika mpango wa kwanza ataruhusiwa kuendelea na mpango wa pili wa Diploma ikiwa atakuwa anaelewa kiingereza vizuri.

Diploma ya Uongozi katika elimu ya Kikristo

Diploma ya Uongozi katika elimu ya Kikristo ni mpango wa miaka mitatu kwa wanafunzi waliohitimu elimu ya Secondary (kozi itakuwa na vipindi 36) yaliyoandaliwa kumwandaa mwanafunzi katika huduma ya Kikristo. kwa wale ambao hawajamaliza elimu ya Secondary wataruhusiwa kujiunga na masomo ya Diploma iwapo watakuwa wamefanya vizuri kwa masomo ya certificate na wawe wanafahamu lugha ya kiingereza vizuri.

Kuhusu sisi

East Africa Christian College (EACC) ni chuo kisicho cha dhehebu, imeunganisha madhehebu ya Kikristo na makao yake makuu yako Tarime, Mara, Tanzania.

EACC imeanzishwa na Wachungaji saba toka madhehebu manne tofauti ya Kikristo hapa Tanzania wakishirikiana na uongozi wa MaxPoint Missions, jumuiya ya kimataifa na shirika la maendeleo la uongozi lenye makao yake makuu Nchini Marekani.

EACC inaongozwa na baraza la viongozi ambao wamechaguliwa na uongozi wa Makanisa shirika yalioanzisha chuo cha EACC.



Inua vipaji vyako vya uongozi kwa kiwango cha juu zaidi



Wasiliana nasi leo

East Africa Christian
College

Phone no +255783586400
Tarime, Mara, Tanzania
www.EastAfricaCC.org

